# JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI - SAME

**FAHARI YA SAME**

**Maendeleo Daima**

**Toleo la Juni 2025 www.samedc.go.tz  email: ded@samedc.go.tz Same DC**

**samedc2022**

# SALAMU KUTOKA KWA MKURUGENZI



***Bw.Jimson Mhagama-Mkurugenzi Mtendaji-Same***

# *Tutunze Mazingira yanayotuzunguka*

***Usafi wa Mazingira suala muhimu kwa jamii yeyote inayohitaji kuwa na afya njema, jamii inayohitaji kuishi bila maradhi na jamii yoyote inayohitaji kuwa na uchumi imara na endelevu.***

***Mazingira yanayotuzunguka yanahitaji jamii yenye kuona umuhimu wa kuhakikisha kuwa mazingira yanakuwa safi,rafiki na mazuri ili kuhakikisha kuwa binadamu na viumbe wengine wanayafurahia.***

***Maradhi mengi ya mlipuko yanatokana na jamii kuishi katika mazingira yasiyofanyiwa usafi wa kutosha na hivyo kuruhusu mazalia ya vijidudu vya magonjwa.***

***Serikali Wilayani Same inatambua umuhimu wa kuishi kwenye mazingira safi imeweka utaratibu mzuri wa kufanya usafi maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwa na gari maalum la kuzolea taka mtaani.***

***Serikali imeelekeza kila mtoa huduma kwa jamii ahakikishe ameweka kifaa maalum cha kunawia mikono kwa maji tiririka.***

***Serikali imetangaza kuwa kika jumamosi ya mwisho wa mwezi lazima wananchi wote wajitokeze kusafisha mazingira yanayowazunguka.***

***Kwa upande wa Serikali imefanya jitihada za kutosha kuhakikisha kuwa wananchi wake wanaishi kwenye mazingira safi japo wapo baadhi ya wananchi wanatupa taka hovyo na hawawekissafi mazingira yanayowazinguka.***

***Kila mkazi ana jukumu la kuhakikisha eneo la mita tano (kila upande) kutoka***

***ilipo nyumba yake linakuwa safi.***

***Wananchi wanapaswa kupeleka taka kwenye gari la taka kila linapopita kwenye maeneo yao.***

***Ni marufuku kutupa taka kwenye mitaro au makorongo na iwapo utapatikana unafanya hivi sheria itachukua mkondo wake.***

***Tukumbuke kuwa Mtu ni Afya na Afya ni Mtaji.***

## KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE BW.ISMAIL ALI USSI ARIDHIA UTEKELEZAJI WA MIRADI SAME.



***Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa 2025 Ndg. Ismail Ali Ussi akizindua Mradi wa Maji Mroyo-Kizangaze.***

Kiongozi wa Mbio za Mwenge Ndg.Ismail Ali Ussi ameelezwa kuridhishwa na utekelezaji wa Miradi nane ya ya Halmashauri ya Wilaya ya Same iliyofikiwa na Mwenge wa Uhuru iliyokuwa na thamani ya shilingi bilioni 2.7.

Akizungumza alipokuwa kwenye uzinduzi wa Mradi wa maji Mroyo-Kizangaze, Maore Wilayani hapa Kiongozi huyo alisema utekelezaji wa Miradi yote iliyofikiwa na Mwenge imefanywa kwa kuzingatia taratibu zote muhimu za Serikali.

"Niwapongeze sana viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same kwa usimamizi mzuri wa Miradi kwani tumekagua Miradi pamoja na nyaraka zake zote na hakuna mashaka yoyote tuliyokutana nayo,hongereni sana" alipongeza Ndg. Ussi.

Akizungumzia mbio za mwenge wa Uhuru Wilayani Same Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni alisema ukiwa Wilayani Same Mwenge wa Uhuru ulizindua Kituo cha Mafuta cha Mayai (Tsh.mil.431) uliweka jiwe la Msingi Zahanati ya Masandare (Tsh.Mil 50.5) ambapo pia ulizindua barabara ya lami Same Mjini yenye urefu wa km 1.43(Tsh.mil.980.9)

Alisema Kiongozi wa mbio za Mwenge Kitaifa Bw. Ismail Ali Ussi alipata nafasi ya kugawa majiko ya gesi 40 kwa wajasiriamali ili kuunga mkono jitihada za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za matumizi ya nishati Safi ya kupikia,majiko hayo yalinunuliwa kwa shilingi milioni 1.9 ambazo zilitokana na mapato ya ndani ya Halmashauri.

Mwenge wa Uhuru pia uliweka jiwe la Msingi kwenye Miradi wa Maji Mroyo-Kizangaze (Tsh.bil 1.1) na kuzindua Nyumba ya Mwalimu Shule ya Sekondari Misufini Goma (Tsh.mil 98.1)

Miradi mingine iliyofikiwa na Mwenge wa Uhuru Kikundi cha Wajasiriamali cha Vijana Welding chenye mtaji wa shilingi milioni 13.

Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru pia alipata fursa ya kugawa viti na meza 200 vyenye thamani ya shilingi milioni 22 kwaajili ya shule za Sekondari.

# DC AIPONGEZA HALMASHAURI YA SAME UKUSANYAJI MAPATO



***Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni***

Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni amewapongeza Watendaji na Madiwani waliomaliza muda wao wa Halmashauri ya Wilaya ya Same kwa kusimamia vyema ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri na kuweza kufikia zaidi ya asilimia 100 ya lengo la kukusanya Bil.3.4 iliyojiwekea kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Ametoa pongezi hizo kwenye kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani ambapo alisema kazi kubwa imefanyika kwenye ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri ambapo Makusanyo yameweza kufikia Bilioni 3.6

"Nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Madiwani, Mkurugenzi na watendaji wengine kwa kazi kubwa mliyofanya ya kusimamia mapato,na tunapouanza mwaka mpya wa fedha hakikisheni mnafikia malengo mliyojiwekea"alisema Mhe.Kasilda

# WANANCHI SAME WAONYWA KUTOJIUNGANISHIA MAJI KWA NJIA ZA ZISIZO RASMI

Wananchi Wilayani Same wameonywa kutotumia njia zisizo rasmi kuunganishiwa huduma ya Maji kwani kufanya hivyo ni kosa kisheria na watakaobainika hatua kali zitachukuliwa dhidi yao.

Onyo hilo limetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Same, Mheshimiwa Kasilda Mgeni, wakati wa kikao cha wadau wa maji kilichoandaliwa na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira (SAMWASA) wilayani Same.

Mhe. Kasilda amesema vitendo vya wizi wa maji vimekuwa kikwazo kikubwa kwa Mamlaka hiyo kufikia malengo ya utoaji wa huduma bora ya maji kwa wananchi.

"Kuharibu miundombinu ya maji au kujiunganishia maji kwa njia ya wizi ni kosa kisheria na ukikutwa utashtakiwa kwa makosa ya uhujumu uchumi"alisema Mhe. Kasilda

Aidha, amewataka wananchi kulipa ankara za maji kwa wakati ili kuwezesha mradi wa maji wa Same -Mwanha-Korogwe (SMK) kujiendesha kwa ufanisi na kuongeza mtandao wa huduma kwa maeneo ambayo bado hayajafikiwa na huduma hiyo muhimu.


Kwa upande wake, Mkurugenzi wa SAMWASA, Mhandisi Rashid Mwinjuma amesema kuwa changamoto ya wizi wa maji inaisababishia mamlaka hiyo hasara kubwa kwa kuikosesha mapato, jambo linalokwamisha juhudi za upanuzi wa huduma kwa wananchi.

Ameeleza kuwa Taasisi hiyo itawachukulia hatua kali za kisheria watumishi wasio waadilifu wanaochangia hasara na kuharibu miundombinu ya maji, huku akitoa wito kwa wananchi kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa za siri pindi wanapobaini vitendo vya ubadhirifu au hujuma dhidi ya miundombinu ya maji.

Sheria ya kuunganisha maji bila kibali ni kosa la jinai linaloweza kusababisha mtu kushtakiwa kwa mujibu wa Sheria ya Uhujumu Uchumi  na pia Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019.

Kwa mujibu wa sheria hizo, mtu yeyote anayejiunganishia maji kinyume cha taratibu, kuharibu miundombinu au kusababisha hasara kwa mamlaka ya maji, anatenda kosa linaloweza kumfikisha mahakamani na kuhukumiwa kwa kosa la jinai, ikiwa ni pamoja na kulipa faini au kifungo jela.

# DC KASILDA AIPONGEZA HALMASHAURI KUTOA MIKOPO YA ASILIMIA 10 KWA WAKATI.




***Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni akikabidhi mfano wa hundi ya malipo kwa vikundi vya wajasiriamali***

Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni ameipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Same kwa kutoa  mkopo wa asilimia 10 za mapato ya ndani kwa wakati ili kuwainua wananchi kiuchumi.

Pongezi hizo zimetolewa na Mkuu wa Wilaya wakati akikabidhi hundi ya Shilingi Milioni 210 ambazo ni Mkopo wa robo ya nne  kwa wanawake ,Vijana na watu wenye ulemavu.

"Nimpongeze Sana Mkurugenzi kwa kuhakikisha kuwa Mkopo huu unatolewa kwa wakati"alisema Mheshimiwa Kasilda

Akizungumza kwenye hafla hiyo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw.Jimson Mhagama amewataka wanufaika wa mkopo kuhakikisha kuwa wanarejesha fedha hizo kwa wakati.

"Serikali imewaamini hivyo hamna budi kuimarisha imani yenu kwa Serikali kwa kurejesha kwa wakati"amesema Mhagama

Kwa upande wake Afisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Same Bw.Anatoly Charles amesema jumla ya vikundi 36 vimenufaika na Mkopo huo ambapo vikundi 24 ni vya wanawake,Vijana ni vikundi 9 na watu watatu wenye ulemavu.

Amesema kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Halmashauri ya Wilaya ya Same imetoa Mkopo wa Shilingi Milioni 585.5 kwa vikundi 113.

## MAFUNZO YATOLEWA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA.



***Baadhi ya Washiriki wa Mafunzo hayo.***

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) Kanda ya Kaskazini imeendesha mafunzo maalum kwa Viongozi wa Serikali kuanzia

ngazi ya Wilaya hadi Vitongoji, Wilayani Same, mkoani Kilimanjaro kwa lengo la kudhibiti matumizi ya madawa ya kulevya.

Mafunzo hayo yaliyofanyika kwenye Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same yalilenga kuwawezesha viongozi hao kutambua, kuzuia na kushughulikia changamoto zinazotokana na matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevya.

Viongozi hao pia wamehimizwa kuzingatia maadili, uwajibikaji na ushirikiano wa kijamii katika mapambano hayo.

Akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Same, Mheshimiwa Kasilda Mgeni, alisema kuwa dawa za kulevya si tu kwamba zina madhara ya kiafya kwa binadamu, bali pia zinachangia kudhoofisha uchumi, kuvuruga familia, kuporomosha maadili, kupunguza nguvu kazi ya Taifa na kuongeza matukio ya uhalifu.

“Hili ni janga linalohitaji nguvu ya pamoja kuanzia kwa viongozi, wazazi, walimu na vijana wenyewe ambao ndio waathirika wakuu wa dawa za kulevya.

Hivyo nawahimiza kupitia mafunzo haya mkawe mabalozi na waelimishaji; muhamasishe na msimamie utekelezaji wa mikakati ya kupambana na dawa za kulevya katika maeneo yenu.”

Aidha, aliwataka viongozi wa serikali kuhakikisha kuwa wanakuwa wawajibikaji, waadilifu na kutofumbia macho biashara haramu ya dawa za kulevya katika maeneo yao.

Kwa upande wake, Afisa Elimu kutoka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Kanda ya Kaskazini Bw. Shaban Miraji, alisema kuwa sababu kuu zinazochangia matumizi ya dawa za kulevya ni pamoja na malezi duni, ukosefu wa elimu sahihi kuhusu madhara ya dawa hizo, pamoja na hali ngumu ya kiuchumi.

Kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya mwaka 2015, mtu yeyote atakayekutwa akilima bangi au mirungi, kufanya biashara, kusafirisha au kumiliki kiasi cha bangi au mirungi kisichozidi kilo 100, atahukumiwa kifungo kisichopungua miaka 30. Iwapo kiasi hicho kitazidi kilo 100, adhabu ni kifungo cha maisha.

# TANESCO YABORESHA UPATIKANAJI UMEME SAME



***Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe.Kasilda Mgeni(katikati)alipotembelea mtambo wa kupoozea umeme wa Maore,kushoto ni Meneja wa Tanesco Same Mhandisi Fabian Ruhumbika.***

Wananchi wa Jimbo la Same Mashariki sasa wanatarajia kupata huduma ya uhakika ya umeme kufuatia ukarabati mkubwa uliofanyika kwenye kituo cha kupokea, kupooza na kusambaza umeme kilichopo Kata ya Maore.

Hayo yamebainishwa na Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Wilaya ya Same, Mhandisi Fabian Ruhumbika wakati Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni alipofanya ziara kukagua ukarabati wa Kituo hicho ambao unagharimu shilingi bilioni 3.3.


Mhandisi Ruhumbika amesema kukamilika kwa mradi huo kutachochea ukuaji wa uchumi kwa wananchi kutokana na kuongezeka kwa uwezo wa umeme kutoka megawati 2 hadi megawati 10.

Mhe. Kasilda amepongeza juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutekeleza Mradi huo ambao ameutaja kama mkombozi wa uchumi wa wananchi.

Serikali imedhamiria ifikapo mwishoni mwa mwaka huu Vijiji vyote hapa nchini viwe vinafikiwa na umeme.

Kwa mujibu wa Taarifa ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020 hadi kufikia Septemba 2024 Jumla ya Vijiji 12,240 Kati ya 12,318 tayari vimeshafikiwa na Umeme ambavyo ni sawa na asilimia 99.37.

# WATUMISHI ZAIDI 1,000 WAPANDISHWA MADARAJA SAME



***Baadhi ya Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same wakiwa kwenye utekelezaji wa majukumu yao.***

Baraza la Madiwani wa Wilaya ya Same limeidhinisha kupandishwa Madaraja kwa watumishi zaidi ya 1,000 wa kada mbalimbali ndani ya Halmashauri ili kuongeza morali na ufanisi kazini.

Akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kabla ya kuvunjwa kwake Juni 20,2025 Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, Mheshimiwa Yusto Mapande, amesema hatua hiyo ni sehemu ya juhudi za kuhakikisha haki na stahiki za watumishi zinalindwa kwa kuzingatia uwajibikaji na utendaji wa mtu mmoja mmoja.

“Tumekuwa tukipima utendaji wa kila mtumishi kwa kuzingatia vigezo halali, watumishi waliopandishwa madaraja wamekidhi vigezo, na tutaendelea kuhakikisha tunatoa motisha kwa wanaojituma kwa bidii kazini,” alisema Mhe.Mapande.

Ameongeza kuwa Halmashauri itaendelea kufanya tathmini ya mara kwa mara kwa watumishi wake ili kuhakikisha ufanisi unabaki kuwa kigezo kikuu cha maendeleo ya taasisi hiyo, huku akisisitiza umuhimu wa maadili na nidhamu kazini.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo Bw.Jimson Mhagama alisema upandishwaji Madaraja Watumishi ni suala endelevu ambalo hufanyika kila mwaka ili kuongeza morali ya kazi.

"Kuwapandisha Watumishi madaraja ni takwa la kisheria lakini pia inawaongezea Watumishi morali ya kufanya kazi"alisema Mhagama.

## WACHIMBAJI MADINI SAME WATAKIWA KUTUNZA MAZINGIRA.




***Afisa Mkazi wa Madini Mkoa wa Kilimanjaro (RMO) Mhandisi Abel Madaha akizungumza kwenye kikao hicho,kushoto ni Mkuu wa Wilaya Mheshimiwa Kasilda Mgeni.***

Wadau wa madini Wilayani Same wametakiwa kuhakikisha kuwa wanatunza Mazingira kwenye maeneo wanayochimba madini kwa kufukia mashimo baada ya kumaliza kuchimba.

Wito huo umetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe.Kasilda Mgeni kwenye kikao cha Wadau wa Madini ya Jasi (Gypsum),Pozolana na Bauxite ambayo hupatikana kwa wingi Wilayani Same ambao wamekutana kujadili changamoto mbalimbali na kuzitafutia ufumbuzi.

Amesema utunzaji wa Mazingira ikiwemo ufukiaji wa mashimo baada ya kuchimba madini ni muhimu kwani itasaidia utunzaji wa maeneo hayo.

"Pamoja na utunzaji wa Mazingira hakikisheni pia mnalipa kwa wakati maduhuli yote ya Serikali ili kukuza uchumi wa nchi"alisema Mkuu huyo wa Wilaya.


Akizungumza kwenye kikao hicho Afisa Mkazi wa Madini Mkoa wa Kilimanjaro (RMO) Mhandisi Abel Madaha amesema uchimbaji Madini umekua ukichangia kwa kiasi kikubwa kwenye pato la Taifa ambapo kwa mwaka 2024/2025 hadi kufikia mwezi April 2025 sekta ya Madini Mkoani humo imekusanya Tsh.Bil.3.2 ambayo ni asilimia 91 ya lengo la kukusanya Tsh.Bil.3.5

Alisema asilimia 31 ya mapato hayo inatokana na mapato ya Madini ya Jasi.

Aliyekuwa Diwani wa Kata ya Makanya ambayo inazalisha kwa wingi Madini ya Jasi Mhe. Damar Kingalu amewaomba wazalishaji wa Jasi kurejesha kiasi cha faida kwa Jamii (CSR) ili kuboresha maisha ya wananchi katika eneo hilo.

Kikao hicho kilichowakutanisha Wadau wa madini ya Jasi zaidi ya 50 wakiwemo wawakilishi wa Viwanda vya Saruji (Moshi,Twiga na Tanga Cement) kimeandaliwa na Tume ya Madini kwa kushirikiana na Chama cha Ushirika wa wachimbaji wa Jasi Mkoa wa Kilimanjaro (Kilimanjaro Gypsum Cooperation Society).

# UTEKELEZAJI MKATABA WA LISHE WAONGEZA IDADI YA WANAFUNZI WANAOKULA SHULENI



***Afisa Lishe Wilaya ya Same Bi.Jackline Kilenga akitoa taarifa ya Hali ya Utekelezaji wa Mkataba wa Afya za Lishe kwenye kikao cha Tathmini ya Mkataba wa Lishe Wilaya.***

Afisa Lishe Wilaya ya Same Bi.Jackline Kilenga amesema idadi ya wanafunzi wanaopatiwa chakula cha mchana shuleni imeongezeka na kufikia asilimia 98.

Aliyasema hayo katika kikao cha tathmini ya utekelezaji wa afua za lishe ambapo alisema afua nyingine zote zilikuwa zikifikia utekelezaji wa asilimia 100 lakini suala la wazazi kuchangia chakula shuleni lilikuwa ni changamoto lakini kwasasa hali ni nzuri.

Amesema kwa upande wa utoaji wa matone ya nyongeza ya vitamin A na utoaji wa dawa za minyoo kwa watoto umefanyika asilimia 128.
Amesema kwa upande wa wajawazito imefanikiwa kuwapatia madini ya chuma na asidi ya foliki kwa asilimia 100.

Bi. Kilenga ametaja shughuli nyingine zilizotelezwa kuwa ni ukaguzi wa maeneo ya vyakula na Elimu ya ulishaji sahihi wa watoto wa changa na wadogo.

Akizungumza baada ya kupokea taarifa hiyo Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni aliwaagiza Watendaji wa Kata kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanapata chakula cha mchana shuleni ili Wilaya ifikie asilimia 100.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw.Jimson Mhagama aliwataka wazazi kutimiza wajibu wao wa kuhakikisha kuwa wanachangia chakula ili kuwawezesha watoto wao kupata mlo wa mchana shuleni.

## DED SAME AIPONGEZA IDARA YA ELIMU KWA USHINDI MNONO UMITASHUMTA




***Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw. Jimson Mhagama (kushoto) akipokea Vikombe vya Ushindi wa UMITASHUMTA toka kwa Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi Mwl.Marclaud Mero, walio pamoja nao ni watumishi wa Idara ya Elimu Msingi (W).***

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw. Jimson Mhagama ameipongeza Idara ya Elimu Msingi Wilayani humo kwa kujinyakulia Vikombe tisa vya Ushindi kwenye Mashindano ya Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) 2025.

Wilaya ya Same ambayo imeshika nafasi ya kwanza kimkoa kwenye mashindano hayo imekabidhi Vikombe tisa vya ushindi kwa Mkurugenzi huyo huku wakiahidi kuendelea kufanya vizuri zaidi.

Akitoa taarifa ya ushindi huo kwa Mkurugenzi, Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi Mwl.Marclaud Mero alisema Wilaya ya Same imeshika nafasi ya kwanza kwenye mchezo wa Riadha , Goalball Wavulana na Sanaa za maonesho.

Aliitaja michezo mingine iliyoitoa Same kimasomaso kuwa ni pamoja na Basketball, Goalball Wasichana na Volleyball wasichana  na wavulana ambazo zilishika nafasi ya pili kimkoa.

Mpira wa Miguu wasichana walishika nafasi ya tatu na Usafi Wilaya ilishika nafasi ya tatu.

Wilaya pia ilifanikiwa kutoa wanamichezo 31 ambao waliunda timu ya Mkoa na iliyokwenda kushiriki Mashindano hayo Ngazi ya Taifa.



***Mkurugenzi pamoja na watumishi Idara ya Elimu wakifurahia Vikombe vya ushindi UMITASHUMTA 2025***

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA




*Vijana wa kikundi cha Maendeleo cha Kata ya Hedaru Wilayani Same wakifurahia mkopo wao wa pikipiki tano uliogharimu Shilingi Milioni 14 fedha ambazo zinatokana na mkopo wa asilimia 10 wa Vijana, wanawake na watu wenye ulemavu*




*Mkuu wa shule ya Sekondari Kisiwani Mwl.Richard Mwita akipokea viti na meza 200 vyenye thamani ya shilingi mil.22 kutoka kwa kiongozi wa mbio za Mwenge 2025 Ndg.Ismail Ali Ussi. Aliyeshika kiti kushoto ni Mkuu wa WIlaya ya Same Mhe.Kasilda Mgeni .*



***Waliokuwa Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Same wakifuatilia kikao cha mwisho cha Baraza kabla ya Baraza hilo kuvunjwa Juni 20,2025***



***Mkuu wa Wilaya ya Mwanga Mheshimiwa Rukia Zuberi akipokea Mwenge wa Uhuru 2025 kutoka kwa Mkuu wa Wssilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni baada ya Mwenge huo kumaliza mbio zake Wilayani Same .***



**JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME**

**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**S.L.P 138,SAME**

**Mhariri Mkuu: Jimson Mhagama**

**Mhariri wa Habari: Amina Sangawe**

***Juni 2025 www.samedc.go.tz  email: ded@samedc.go.tz Same DC samedc2022***